# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.11 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JANUARI 2022

# WAZIRI UMMY AMWAPISHA WAKILI MRINA KUWA KAMISHNA WA TSC



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kushoto) akimwapisha Wakili Optat James Mrina kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Uapisho huo umefanyika Novemba 30 katika ofisi ya Waziri huyo jijini Dodoma.*

**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu:** +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz **Tovuti:** www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

## MWAKA 2022 UWE WA MAFANIKIO ZAIDI KATIKA KUTOA HUDUMA KWA WANAFUNZI

Ni wazi kwamba mwaka 2021 walimu wamefanya kazi kubwa katika kukuza elimu yetu hapa nchini. Tukiangalia viwango vya ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari vimekuwa vikiongezeka kutokana na kazi kubwa inayofanywa na walimu.

Ukiachilia mbali kufundisha darasani, walimu pia wamekuwa na shughuli za usimalizi wa miradi mbalimbali ya shule ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea nchi nzima baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuelekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ikiwa ndiyo chombo kinachoshughulikia walimu katika masuala ya Ajira na Nidhamu, tunaridhishwa na kazi kubwa inayofanywa na walimu, japokuwa zipo dosari za hapa na pale kwa walimu wachache kutozingatia maadili ya kazi na kujikuta wamechukuliwa hatua za kinidhamu.

Mwaka 2021 pia umekuwa wa neema kwa watumishi wa Umma wakiwemo walimu baaya ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kusikia kilio muda mrefu cha kutopandishwa madaraja watumishi na kuamua watumishi wote wenye sifa za kupandishwa madaraja wapandishwe. Kutokana na agizo hilo TSC ilipandisha walimu wote waliostahili ambao idadi yao ni 126,346. Kwa hili tuna kila sababu ya kuipongeza na kuishukuru Serikali yetu kwa kumaliza kero hiyo.

Tayari tumeingia mwaka mwingine 2022 ambapo sasa kwa upande wa walimu wanaweka malengo ya kazi ambazo watazitekeleza kwa mwaka mzima. Kila mwalimu hana budi kuweka malengo yake kwa mujibu wa taratibu na mwisho wa mwaka utendaji wake wa kazi utapimwa kwa kuzingatia malengo hayo.

Wito wetu kwa walimu ni kuhakikisha wanaendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na ubunifu ili tuendelee kupata mafanikio zaidi.Tabia za kutohudhuria darasani wakati wa vipindi, kuingia darasani bila kufundisha, kufundisha bila kuzingatia nyenzo za kazi na kila aina ya uvunjifu wa Maadili ya Kazi ya Ualimu tuviepuke.

Kheri ya mwaka mpya 2022.

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

### KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Kheri ya
Mwaka Mpya
2022
Mwenyekiti, Katibu, Wajumbe, Menejimenti na Watumishi wa TSC wanawatakia Watanzania wote Kheri ya Mwaka Mpya 2022
“Tunawapongeza Walimu wetu kwa kazi kubwa mliyoifanya mwaka 2021 katika kuwahudumia Wanafunzi.Tuna imani kuwa mwaka huu 2022 tutaendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu na ubunifu zaidi ili kuongeza mafanikio kwenye Sekta ya Elimu”
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania
Tumeyautumishiwawalimu

# WAZIRI UMMY AMWAPISHA WAKILI MRINA KUWA KAMISHNA WA TSC



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kushoto) akimwapisha Wakili Optat James Mrina kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Uapisho huo umefanyika Novemba 30 katika ofisi ya Waziri huyo jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu amemwapisha Wakili, Optat James Mrina kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Uapisho huo umefanyika Novemba 30, 2021 katika Ofisi za Waziri Ummy jijini Dodoma ambapo Waziri huyo alimkaribisha Kamishna Mrina kujiunga na TSC kumuasa kufanya kazi kwa bidii na weledi ili TSC iendelee kutoa huduma bora kwa walimu.

Waziri Ummy alisisitiza kuwa TSC ni chambo muhimu kinachotegemewa na Serikali katika kusimamia Ajira, Nidhamu na maendeleo ya walimu nchini hivyo makamishna wa tume hiyo ni lazima wawe ni watu makini katika kuamua masuala mbalimbali ya ofisi hiyo.

Mara baada ya uapisho huo, Mrina alifika ofisi za TSC na kukaribishwa na Katibu wa Tume hiyo, Paulina Nkwama ambaye alieleza kuwa uteuzi wa kiongozi huyo umefanyika wakati muafaka kwani TSC ina uhitaji mkubwa wa utaalamu wa wanasheria katika kuamua rufaa za walimu.

Nkwama alimweleza Kamishna huyo kuwa kuwa TSC inahudumia jumla ya walimu 258,290 wanaofundisha shule za msingi na sekondari za serikali ambapo katika idadi hiyo walimu 173,591 ni wa shule za msingi na walimu 84,700 ni wa shule za sekondari.

Aliongeza kuwa TSC imekuwa ikijitahidi kuhakikisha walimu wanahudumiwa vizuri na wanatendelewa haki katika masuala mbalimbali ya utumumishi wao, hivyo anaamini kuwa kuteuliwa na kuapisha kwa



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kushoto) na Kamishna wa TSC Wakili Optat James Mrina wakisaini kiapo ambacho Waziri Ummy alimwapisha Kamishna Mrina.*

# WAZIRI UMMY AMWAPISHA WAKILI MRINA KUWA KAMISHNA WA TSC



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (aliyekaa mbele) akiwa pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakimkaribisha Kamishna mpya wa TSC, Wakili Optat James Mrina (wa kwanza upande wa kulia) mara baadya ya kuwasili kwenye ofisi za TSC Novemba 30, 2021.*

wakili Mrina kutaongeza chachu kwa TSC kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Naye Wakili Mrina alimshukuru Katibu wa TSC kwa jitihada zake alizofanya kufanikisha hafla hiyo ya kuapishwa kwake huku akiahidi kuwa atatumia uwezo wake wote katika kuhakikisha tume hiyo inapiga hatua zaidi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Mrina ameteuliwa na kuapishwa kuchukuwa nafasi ya Wakili Paul Shahidi ambaye alipata uhamisho na kuhama kutoka Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali. Kwa mujibu wa Sheria ya TSC Na. 25 ya Mwaka 2015 Makamishna wa Tume wanatoka katika ofisi mbalimbali za Serikali.

Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi pamoja wajumbe wawili wanaowakilisha Chama cha Walimu ambapo mmoja anawakilisha shule za msingi na mwingine shule za sekondari.

Hivyo, pale ambapo mjumbe/Kamishna anapata uhamisho na kuhamia ofisi nyingine, anapoteza sifa ya kuendelea kuwa Kamishna wa TSC na ndiyo sababu Waziri Ummy alimteua Wakili Mrina kujaza nafasi iliyokuwa wazi.



*Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo (kulia) akimkabidhi Kamishna mpya wa TSC, Wakili Optat James Mrina kitabu chenye Sheria na Kanuni za TSC ikiwa ni ishara ya kumkaribisha katika kutekeleza majukumu ya TSC.*

# WALIMU TULIWEZESHE TAIFA KUWA NA WATU WENYE MAADILI KWA KUSIMAMIA VEMA ELIMU MSINGI NA SEKONDARI – NKM MWELI



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli akizungumza wakati wa kufungua Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi yaliyofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli, ametoa wito kwa walimu wote nchini kuwa chachu ya kuliwezesha Taifa kuwa na watu wenye maadili kwa kutekeleza na kusimamia vema elimu ya msingi na sekondari kama Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na maadili katika Utumishi wa Umma zinavyoelekeza.

Alisema kwa takwimu zilizopo hadi kufikia mwezi Oktoba, 2021 Taifa lina jumla ya walimu 258,291 ambapo kati yao 173,591 ni walimu wa shule za msingi na 84,700 wa shule za sekondari wanaohudumiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu, hivyo Kamati za Tume za Wilaya zina wajibu wa kuhakikisha walimu wanapata huduma zinazostahili na kupunguza malalamiko na changamoto mbalimbali miongoni mwao.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu huyo alipokua Mgeni Rasmi akimuwakilisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, OR – TAMISEMI, Ummy Ally Mwalimu (Mb), alipokua akifungua Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe,



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli akizungumza wakati wa kufungua Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi yaliyofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma.*

# WALIMU TULIWEZESHE TAIFA KUWA NA WATU WENYE MAADILI KWA KUSIMAMIA VEMA ELIMU MSINGI NA SEKONDARI – NKM MWELI



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC), Willy Komba akitoa maneno ya kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli ili afungue Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi yaliyofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma.*

Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi yaliyofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma.

"Moja ya madhumuni ya Mafunzo haya Elekezi kwenu Wajumbe Wateule wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) nchini, ni kusaidia kuendeleza dhamira ya dhati ya Serikali yetu katika kusimamia kwa vitendo dhana ya misingi ya uadilifu, kuimarisha nidhamu katika Utumishi wa Walimu na kuongeza kasi ya maendeleo ya elimu kwa Taifa." Alisema Naibu Katibu Mkuu Mweli

Pamoja na hilo alisema jingine ni kusaidia kuzikumbusha na kuzihamasisha kamati hizo kuhusiana na wajibu na



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*

mamlaka zao za nidhamu kwa ajili ya kutenda haki wakati wa kushughulikia masuala ya walimu yahusuyo ajira, miiko, maadili, na nidhamu katika kazi zao.

Aidha, amewapongeza sana wajumbe wote wateule kwa kuweza kutekeleza majukumu yao vema kwa kipindi chote tangu kuteuliwa mwezi Mei, 2020 mpaka kupata mafunzo mwezi Desemba, 2021 ambapo Serikali sasa inaamini baada ya mafunzo hayo wajumbe watatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Vilevile, Naibu Katibu Mkuu Mweli aliuagiza Uongozi wa Tume kuhakikisha mafunzo hayo yanakua endelevu kwa wajumbe

# WALIMU TULIWEZESHE TAIFA KUWA NA WATU WENYE MAADILI KWA KUSIMAMIA VEMA ELIMU MSINGI NA SEKONDARI – NKM MWELI



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*

wote kila wanapoteuliwa na kukamilisha kwa wajumbe wa kamati za wilaya zote ambazo bado hazijapatiwa mafunzo hayo huku Serikali kupitia OR-TAMISEMI ikiahidi kuhakikisha inatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa mafunzo hayo siku zijazo.

Alisema, "Wajumbe wote mnaoshiriki katika mafunzo haya mna mchango mzuri wa mawazo ambao utawezesha kuweka mikakati mizuri ambayo itatumika kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kila siku wa majukumu yenu na itasaidia Tume pia kusimamia vyema maadili ya walimu na kuchukua hatua stahiki kwa walimu watakaobainika kukiuka maadili na miiko ya kazi yao."

Kabla ya kufungua rasmi mafunzo hayo aliwaomba wajumbe wa kamati katika maeneo yao kuendelea na uhamasishaji na kushiriki kikamilifu katika zoezi la sensa litakalofanyika mwakani 2022, kwani itasaidia katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali.

Kuhusiana na janga kubwa la UVIKO-19 lililoikumba nchi yetu na dunia kwa ujumla tangu mwaka 2019, alitoa rai kwa washiriki kujitoa kwa hiyari katika kuchanja ili kuendelea kuimarisha zaidi kinga za miili na kuwalinda wengine tunaojumuika nao katika maeneo mbalimbali.

Nae Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba, alisema tangu kuanzishwa kwa Tume na kuanza kutekeleza majukumu yake mwezi Julai, 2016 Tume imetimiza miaka mitano na miezi sita huku muda uliowekwa Kisheria kwa wajumbe wa Tume na Kamati za Wilaya ni miaka mitatu. Hivyo, Tume iliyopo sasa pamoja na Kamati za Wilaya niza awamu ya pili, baada ya wajumbe wa awali kukamilisha muda wao.

# KAMATI ZA TSC WILAYA ZINA WAJIBU WA KUHAKIKISHA WALIMU WANAPATA HUDUMA ZINAZOSTAHILI NA KUPUNGUZA MALALAMIKO NA CHANGAMOTO MIONGONI MWAO



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli, ameainisha kuwa hadi kufikia mwezi Oktoba, 2021 Taifa lina jumla ya walimu 258,291 ambapo kati yao 173,591 ni walimu wa shule za msingi na 84,700 wa shule za sekondari wanaohudumiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu, hivyo Kamati za Tume za Wilaya zina wajibu wa kuhakikisha walimu wanapata huduma zinazostahili na kupunguza malalamiko na changamoto mbalimbali miongoni mwao.

Aidha, alitoa wito kwa walimu wote nchini kuwa chachu ya kuliwezesha Taifa kuwa na watu wenye maadili kwa kutekeleza na kusimamia vema elimu ya msingi na sekondari kama Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na maadili katika Utumishi wa Umma zinavyoelekeza.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu huyo alipokua Mgeni Rasmi akimuwakilisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, OR – TAMISEMI, Ummy Ally Mwalimu (Mb), alipokua akifungua Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi yaliyofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma.

"Nawapongeza sana wajumbe wote wateule kwa kuweza kutekeleza majukumu yao vema kwa kipindi chote tangu kuteuliwa mwezi Mei, 2020 mpaka kupata mafunzo mwezi huu wa



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*

# KAMATI ZA TSC WILAYA ZINA WAJIBU WA KUHAKIKISHA WALIMU WANAPATA HUDUMA ZINAZOSTAHILI NA KUPUNGUZA MALALAMIKO NA CHANGAMOTO MIONGONI MWAO

Desemba, 2021 ambapo Serikali sasa inaamini baada ya mafunzo haya wajumbe wote mtatekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi." Alisema Naibu Katibu Mkuu (Elimu)

Vilevile, Naibu Katibu Mkuu Mweli aliuagiza Uongozi wa Tume kuhakikisha mafunzo hayo yanakua endelevu kwa wajumbe wote kila wanapoteuliwa na kukamilisha kwa wajumbe wa kamati za wilaya zote ambazo bado hazijapatiwa mafunzo hayo huku Serikali kupitia OR-TAMISEMI ikiahidi kuhakikisha inatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa mafunzo hayo siku zijazo.

Alisema, "Wajumbe wote mnaoshiriki katika mafunzo haya mna mchango mzuri wa mawazo ambao utawezesha kuweka mikakati mizuri ambayo itatumika kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kila siku wa majukumu yenu na itasaidia Tume pia kusimamia vyema maadili ya walimu na kuchukua hatua stahiki kwa walimu watakaobainika kukiuka maadili na miiko ya kazi yao."

Nae Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba, alisema tangu kuanzishwa kwa Tume na kuanza kutekeleza majukumu yake mwezi Julai, 2016 Tume imetimiza miaka mitano na miezi sita huku muda uliowekwa Kisheria kwa wajumbe wa Tume na Kamati za Wilaya ni miaka mitatu. Hivyo, Tume iliyopo sasa pamoja na Kamati za Wilaya niza awamu ya pili, baada ya wajumbe wa awali kukamilisha muda wao.

Hali kadhalika, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, pia aliwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wateule wa kamati za wilaya kwa ushirikiano wao na kujitahidi kutekeleza majukumu yao vema licha ya kuwa na majukumu mengine wakiwa pia ni watumishi wa umma katika ofisi zao nje ya majukumu ya Tume na kuwaomba waendeleze moyo huo wa Kizalendo.

Sehemu ya mada zilizowasilishwa katika mafunzo haya ni pamoja na; kusudi la kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, Muundo na Majukumu ya Tume, Majukumu ya Tume kuhusu masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Maadili/ Miiko ya Kazi ya Ualimu, Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu na Taratibu za Uendeshaji wa vikao vya Kamati za Wilaya.



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli akiagana na Mwenyekiti wa TSC Prof. Willy Komba mara baada ya Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi yaliyofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma. Wengine ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kulia) pamoja na viongozi wengine kutoka TSC.*

# WALIMU WAOMBA SERIKALI KUUNDA CHOMBO KIMOJA KITAKACHOSHUGHULIKIA MASUALA YOTE YA WALIMU KWA PAMOJA KATIKA UTUMISHI WAO KWA UMMA

**Na. Mwandishi Wetu – Iyunga, Mbeya**



*Mwenyekit wa TSC, Prof. Willy Komba akiongea na Walimu (hawapo pichani) mkoani Mbeya. Wengine ni viongozi wa TSC walioambatana na mwenyekiti huyo.*

Walimu mkoani Mbeya wameiomba Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (TSC) kuunda chombo kimoja kitakachowahudumia walimu wote nchini kwa kushughulikia masuala yao mbalimbali kuanzia ajira, mishahara, malimbikizo ya madeni mbalimbali, upandishwaji vyeo na madaraja, ubadilishaji kada wakiwa kazini, na masuala mbalimbali ya nidhamu na maadili kazini katika Utumishi wa Walimu na Umma kwa ujumla wake.

Rai hiyo ilitolewa hivi karibuni wakati wa Kikao Kazi baina ya walimu hao na na baadhi ya Makamishna wa TSC wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tume Prof. Willy Komba mara baada ya Mkutano wa Tume wa Robo ya Pili kumalizika, kikao kilichofanyika katika Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga mkoani humo kwa lengo la kukumbushana baadhi ya mambo muhimu katika utumishi wa walimu ikiwa ni pamoja na kukumbushwa Historia na Majukumu ya TSC kwa walimu, Nguzo Kuu Tano za Ualimu, pamoja na masuala ya nidhamu na maadili kazini.





*Baadhi ya Walimu waliohudhuria kikao.*

"Moja ya vyombo vinavyosaidia walimu kwa karibu sana katika kutatua changamoto mbalimbali tunazokumbana nazo kiutumishi tangu kuajiriwa ni TSC. Hivyo, kutokana na uwepo wa vyombo kadhaa vinavyotuhudumia walimu na kufanya walimu wengine kutojua jambo gani linatakiwa kwenda wapi na liupi liende wapi baina ya vyombo hivyo, tunaiomba TSC kupitia Wizara Mama (TAMISEMI) na Wizara ya Elimu; kwanza itusaidie kupata chombo kimoja kitakachotuhudumia katika kila hitaji letu kuanzia tunapoajiriwa,

# WALIMU WAIOMBA SERIKALI KUUNDA CHOMBO KIMOJA KITAKACHOSHUGHULIKIA MASUALA YOTE YA WALIMU KWA PAMOJA KATIKA UTUMISHI WAO KWA UMMA

lakini pili Serikali iangalie namna ya kuongeza bajeti ya TSC kushughulikia majukumu yake na masuala ya walimu kwani hii itaisaidia TSC kutufikia walimu wote kwa urahisi zaidi nakwa wakati na kutupatia elimu na ufumbuzi wa haraka kwa yale yanayotukabili tuwapo katika vituo vyetu mbalimbali vya kazi hapa nchini." Alisema Mwl. Nelusiwe Kayuni ambaye ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Iwambi kwa niaba ya walimu waliohudhuria kikao hicho

Pamoja na rai hiyo Mwl. Kayuni aliiomba TSC kuendeleza ufuatiliaji wa karibu wa uteuzi na uthibitishwaji wa Katibu Wasaidizi wa TSC Wilayani ili kuwapa mamlaka na nguvu zilizo kamili katika kuwahudumia lakini pia kuwapa ujasiri zaidi wa kuwa na sauti ya kimaamuzi kwa walimu wanaowahudumia ndani ya wilaya 139 wanazozisimamia hapa nchini huku akitoa shukrani na kuzipongeza Halmashauri ya Wilaya na ile ya Jiji la Mbeya kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya TSC Wilaya katika kufanikisha zoezi la upandishaji vyeo walimu waliostahili kupandishwa na kubadilishiwa mishahara yao kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

Aidha, akijibu maswali na hoja mbalimbali za walimu katika kikao hicho hasa kuhusiana na usajili wa walimu wa masomo ya ufundi ambao hawana sifa za ualimu Mkurugenzi wa Ajira, Nidhamu na Maendeleo ya Walimu Mwl. Christina Hape alisema, "Serikali inatambua kuna walimu wapatao 150 ambao hawajasajiliwa kutokana na kukosa sifa ya kuwa walimu na hiv



*Mwenyekit wa TSC, Prof. Willy Komba (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Walimu wa Shule ya Msingi na Sekondari wa Mkoa wa Mbeya waliohudhuria Kikao Kazi kilichowakutanisha na Viongozi wa TSC. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika Shule ya ya Sekondari ya Ufundi Iyunga mkoani humo. Wengine ni viongozi wa TSC walioambatana na mwenyekiti huyo.*

Tume na Wizara Mama inaandaa mafunzo kwa ajili ya walimu hao kujengewa uwezo na kuwa na sifa ya ualimu ili baada ya mafunzo hayo waweze kusajiliwa moja kwa moja kama walimu kamili."

Nao Makamishna wa TSC, Mwl.Joyce Mtindya na NACTE katika majumuisho wameuomba Uongozi wa TSC kutoa elimu zaidi juu ya utaratibu wa kukata rufaa za mashauri ya nidhamu katika ngazi zote na kufanya uchambuzi wa sababu zinazopelekea utoro wa walimu katika vituo vyao vya kazi ili kupunguza au kuondoa kabisa idadi ya rufaa zinazopokelewa nje ya muda, kupunguza asilimia ya rufaa zinazoelekezwa kurudiwa upya kwa makosa yanayoepukika ikiwa ni pamoja na kuona namna sahihi ya kupunguza au kuondoa kabisa utoro.

Akihitimisha Kikao hicho Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba, *Baadhi ya Walimu waliohudhuria kikao.*mishi wowote iwe ajira rasmi ya Serikali au Binafsi ni lazima kutimiza wajibu ili kupata motisha au kupanda cheo. Hivyo, kuwasihi walimu kutofadhaika na kauli za kupanda cheo ni haki au zawadi kwani haki na zawadi hupatikana baada ya wajibu fulani kutekelezwa na kuwataka kuendelea kuchapa kazi ikiwa ni sehemu ya wajibu ili kupata motisha kiutendaji.

Katika Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu wa Robo ya Pili ya Utekelezaji wa Mwaka wa Fedha 2021/2022; jumla ya rufaa za nidhamu na maadili 45 zilitolewa, ambapo kati ya hizo rufaa 15 zilikubaliwa, rufaa tisa zilielekezwa na Tume kuanza kusikilizwa upya, rufaa 22 zilikataliwa, na rufaa tisa zilitupiliwa mbali kwasababu mbalimbali ikiwemo kuwasilishwa nje ya muda unaotakiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu,.

# TSC Yapandisha Madaraja Walimu 126,346



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea na washiriki (hawapo pichani) wakati wa kufunga Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kwa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi wetu.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amesema tume hiyo kupitia Kamati zake za Wilaya imefanikiwa kuwapandisha vyeo/madaraja walimu 126,346 wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali katika zoezi la upandishaji vyeo liliofanyika mwezi Juni 2021.

Katibu huyo ameyasema hayo wakati akieleza mafanikio ya TSC katika kipindi cha kunzia Julai 2020 hadi Novemba 2021 wakati wa kufunga mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kwa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Amesema zoezi hilo lililofanyika kwa mafanikio makubwa lilihusha upandishaji vyeo walimu kwa ikama ya miaka mitatu mfululizo ambayo ni 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 kwa mujibu wa maelekezo kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

"Miongoni mwa mafanikio ya TSC katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi sasa ni kupandisha vyeo walimu 126,346. Hili lilikuwa zoezi la kihistoria kwa sababu walimu wote waliokuwa wamestahili kupanda tuliwapandisha na tumehakikisha hakuna aliyekuwa na sifa za kupanda ambaye aliachwa, alisema.

Kiongozi huyo alieleza kuwa katika zoezi hilo, watumishi waliopandishwa madaraja walibadilishiwa mishanara yao mapema kitu ambacho kimeondoa malimbikizo ya madeni ya mishahara yalikuwa yakilalamikiwa kipindi cha nyuma.

Nkwama alieleza pia kwamba TSC imefanikiwa kuandaa miongozo ya wakuu wa shule katika kusimamia masuala ya Maadili na Nidhamu pamoja na



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea na washiriki wakati wa kufunga Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kwa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# TSC Yapandisha Madaraja Walimu 126,346



*Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo akiwasilisha mada wakati Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kwa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

Ajira na Maendeleo ya Walimu shuleni huku akisisitiza Kamati za Wilaya kuhakikisha walimu wanaipata miongozo hiyo.

"Kwanza napenda Wajumbe wa Kamati zote za Wilaya waisome na kuielewa miongozo hii lakini pia mtusaidie kuhakikisha inafika kwa walimu, nao waisome na kuielewa ili msuala yote ya walimu yashughulikiwe kwa mijibu wa sheria, kanuni na taratibu," alisema.

Kwa upande wa mashauri ya nidhamu ya walimu, Katibu huyo alieleza kuwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Novemba 2021 jumla ya mashauri 1979 yalishughulikiwa ambapo mashauri 1036 yalihusu utoro, 502 yalihusu kughushi vyeti na mashauri 441 yalihusu makosa mbalimbali yakiwemo ulevi, mapenzi na wanafunzi na kutotii mamlaka.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho, rufaa 208 zilizopinga umamuzi uliotolewa na TSC ngazi ya Wilaya zilikatwa kwa Tume Makao Makuu kwa mujibu wa sheria ya TSC Sura 448 huku akieleza kuwa hakuna rufaa iliyokatwa kupinga uamuzi uliofanyika katika ngazi ya shule.

Alieleza kuwa kutokatwa rufaa huko katika ngazi ya shule huenda kunatokana na walimu kutofahamu sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Walimu kitu ambacho wakati mwingine kinaweza kuwanyima haki haki yao ya msingi.

"Tuendelee kutoa elimu ya kutosha ili kila mwalimu atambue wajibu na haki zake. Pale ambapo itatokea mwalimu hataki kufuata maadili ya kazi yake kwa mujibu wa sheria, basi sheria ichukue mkondo wake na haki iweze kutendeka, lakini mhusika naye awe anajua na atumie haki yake kikamilifu," alisema.

Mafanikio mengine aliyoeleza ni kutoa mafunzo kwa Kamati za Wilaya katika Kanda 5 kati ya 7 ambapo wahusika walipatiwa uelewa wa masuala mbalimbali yanayohusu Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 pamoja na kanuni zake za mwaka 2016.

"Lengo letu ni kuhakikisha mwaka huu wa fedha tunazifikia kanda zote na kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ili wanapoendelea kutekeleza majukumu yao wawe na uelewa wa kutosha, na haki iweze kutendeka," alisema Nkwama.



*Badhi ya washiriki wa Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kwa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa mafunzo.*

# CWT IRINGA YAIPONGEZA SERIKALI, UPANDISHAJI MADARAJA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu.**

Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Iringa kimeipongeza Serikali kwa kuendesha zoezi la upandishaji na ubadilishaji vyeo walimu kwa ufanisi kitu ambacho kimefanya kupungua kwa malalamiko na kero za walimu zilizodumu kwa muda mrefu.

Hayo yamesememwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Iringa, Genovefa Barnabas wakati Jarida la Sauti ya TSC lilipofika ofisini kwake kwa lengo la kupata habari za Utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Genovefa Barnabas akiwa ofisini kwake wakati wa mahojiano maalaum na Jarida hili.*

Kiongozi huyo alisema kutokana na zoezi la kupandisha madaraja walimu kwenda vizuri pamoja na ushirikiano wanaoupata kutoka serikalini, CWT mkoani hapo waliamua kufanya kikao na wadau wa elimu na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhudumia walimu.

"CWT walituita na lengo kubwa ilikuwa kuishukuru Serikali kutokana na zoezi la upandishaji madaraja na ubadilishaji wa vyeo walimu lilivyokwenda vizuri. Vile vile wameipongeza Serikali kutokana na ushirikiano wanaoupata pale wanapokuja kwetu kwa masuala ya walimu. Kwa kweli tulifarijika kuona kwamba juhudi za Serikali chini ya Uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan za kuboresha maslahi ya watumishi wakiwemo walimu zimekuwa na mafanikio makubwa," alisema.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akiandika jambo wakati wa mahojiano yake na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Genovefa Barnabas. Mahojiano hayo yamefanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Wilaya ya Iringa.*

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alifafanua kuwa zoezi la upandishaji vyeo watumishi wa Umma lililofanyika mwezi Juni, 2021 lilikwenda vizuri na ofisi yake ilipandisha jumla ya walimu 1566 na kuwabadilishia muundo walimu 196 jambo ambalo hakuwahi kulishuhudia katika historia yake ya kuwahudumia walimu.

"Katika historia yangu ya utumishi wa umma tangu nimeanza kuhudumia walimu sijawahi kuona promotion kama za mwaka huu. Tulifanya kazi usiku na mchana kufanikisha zoezi hili na matunda yake tumeyaona. Idadi kubwa ya walimu wamepanda na kupata mishahara mipya kwa wakati kitu ambacho kimeondoa malimbikizo ya madeni ya watumishi," alisema.

Kwa mujibu wa Genovefa,

# CWT IRINGA YAIPONGEZA SERIKALI, UPANDISHAJI MADARAJA WALIMU

wapo walimu wanaofika ofisini kwake wakiwa na changamoto za kiutumishi huku wengi wao wakiwa na madai ya kucheleweshwa kupanda daraja kwa miaka ya nyuma na wengine kucheleweshwa kubadilishiwa cheo, na kwa kushirikiana na waajiri wamekuwa wakiwaombea vibali vya kuwapandisha na kuwabadilishia cheo kutoka kwa Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

"Tunamshukuru sana Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa sababu amekuwa akitoa vibali vya kupandisha walimu mmoja mmoja kulingana na kesi husika, nayeye amekuwa akitoa vibali kwa wakati kitu ambacho kimeendelea kuwasaidia sana walimu," alisema Genovefa.

Akizungumzia hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo, Geonovefa alisema katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, 2021 jumla ya mashauri matano yalifunguliwa ambapo mawili kati ya hayo yamehitimishwa na mashauri matatu yanaendelea kushughulikiwa.

Ameeleza kuwa pamoja na kuwa inadi ya mashauri yanayofunguliwa yamepungua kwa kiasi kikubwa, ofisi yake haiwezi kusema kuwa hakuna walimu kwenye Wilaya hiyo wenye tabia za utovu wa nidhamu kwa kile anachokiona kuwa yapo masula ya utovu wa nidhamu yanayosikika mtaani lakini hayafikishwi ofisini kwake.

"Tukiangalia idadi ya mashuri tunayowafungulia walimu tunaweza kusema hali ya nidhamu kwa walimu ni nzuri sana. Lakini ukweli ni kwamba yapo mambo ambayo yanasikika mitaani lakini hayaletwi kwetu. Mara nyingi unakuta yanamalizwa kienyeji huko mtaani, hivyo hata ukitaka kufuatilia hupati ushirikiano kutoka kwa jamii," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo amesema kuwa ofisi yake inaendelea kujikita katika kutoa elimu kwa walimu ili kuhakikisha wanazingatia Maadili na Miiko ya Kazi yao wakati wakiwa shuleni na nje ya shule.

TSC Wilaya ya Iringa inasimamia walimu katika Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Iringa yenye walimu 1404, shule za msingi 43 na sekondari 16 pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa yenye walimu 2114, shule 148 za msingi na 31 za sekondari za Serikali.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akimsikiliza Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Iringa, Genovefa Barnabas (kulia) katika mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Iringa.*



*Picha ya jengo la TSC Wilaya ya Iringa*

# WATUMISHI WA TSC KATIKA WILAYA ZA MKOA WA MARA WAHIMIZWA KUSIMAMIA KIKAMILIFU MAADILI NA NIDHAMU KWA WALIMU

**Na mwandishi wetu, Mara.**

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika Wilaya za Mkoa wa Mara wamehimizwa kusimamia kikamilifu Maadili na Nidhamu kwa walimu wa Mkoa huo.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Tarime Mhe. Luteni Gabriel Mntenjele wakati akifungua kikao kazi cha watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara kilichofanyika tarehe 08/12/2021 katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Blue Sky iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Tarime ikiwa ni utaratibu waliojiwekea watumishi hao wa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka kwa ajili ya kujadili na kujengeana uwezo katika masuala ya utekelezaji wa majukumu yao pamoja na ustawi wao.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho Mhe. Mntenjele alisema,"Nawashukuru wana TSC Mkoa wa Mara kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika kikao kazi hiki. Binafsi ni mwalimu kitaaluma na kauli mbiu ya chuo nilichosoma ilikuwa ni mwalimu kwa mfano, yaani mwalimu anapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika jamii,: alisema.

Aliendelea kusema kuwa,"Hata hivyo, hali ilivyo sasa kuna baadhi ya walimu wanakiuka Maadili ya kazi ya Ualimu ikiwa ni pamoja na kuvaa mavazi yasiyo rasmi kama watumishi wa Umma, unywaji wa pombe kupindukia, utoro kazini, uzembe wa kutofundisha na wengine wanajihusisha kimapenzi na wanafunzi. Hivyo, ninyi Tume ndiyo dawati zuri la kudhibiti na kusimamia Maadili na Nidhamu ya walimu wetu. Tumieni kikao kazi hiki kuhakikisha mnajadili namna ya kusimamia vema Maadili na Nidhamu za walimu katika Mkoa wetu na kuhakikisha walimu wanarudi kwenye mstari."

Aidha Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kushughulikia kero za watumishi hususani walimu kwa kuwapandisha vyeo pamoja na kuajiri walimu wapya mwanzoni mwa mwezi Julai, 2021 na kutoa wito kwa walimu na watumishi wengine kuonesha fadhila kwa Serikali kwa kufanya kazi kwa bidii.

"Wahimizeni walimu wetu wafanye kazi kwa bidii ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi wanaowafundisha ili kuonesha fadhila kwa Rais wetu mpendwa Mhe. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali anayoiongoza, maana hatua alizochukua za kupandisha watumishi vyeo na kuajiri walimu wapya zimesaidia kupunguza malalamiko miongoni



*Kaimu Katibu Msaidizi Wilaya ya Tarime Bw. Julius Agutu (aliyesimama) akitoa maelezo ya kumkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Tarime Mhe. Luteni Gabriel Mntenjele (aliyekaa kiti cha mbele katikati) aliyekuwa Mgeni Rasmi katika kikao kazi cha watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara kilichofanyika tarehe 08/12/2021 Mjini Tarime. Wengine walioketi ni baadhi ya watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara.*



*Baadhi ya Watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara wakiwa katika Picha ya Pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Tarime Mhe. Luteni Gabriel Mntenjele (aliyekaa kiti cha mbele katikati) aliyekuwa Mgeni Rasmi katika kikao kazi cha watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara kilichofanyika tarehe 08/12/2021 Mjini Tarime.*

# WATUMISHI WA TSC KATIKA WILAYA ZA MKOA WA MARA WAHIMIZWA KUSIMAMIA KIKAMILIFU MAADILI NA NIDHAMU KWA WALIMU

mwa walimu na watumishi wengine" alisema Mkuu huyo wa Wilaya ya Tarime.

Awali akimkaribisha Mkuu huyo wa Wilaya ya Tarime, Kaimu Katibu Msaidizi wa Wilaya ya Tarime Bw. Julius Agutu ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa wana TSC Mkoa wa Mara alieleza kuwa hicho ni kikao kazi Na. 01/2021/2022 cha watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara ikiwa ni utaratibu waliojiwekea wa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka.

"Mhe. Mgeni Rasmi, napenda kukujulisha kuwa hiki ni kikao kazi Na. 01/2021/2022 cha sisi watumishi wa Tume kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara ikiwa ni utaratibu tuliojiwekea wa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka, lengo likiwa ni kujadili namna bora ya utekelezaji wa majukumu yetu, kufahamiana na kujadili masuala ya ustawi wetu" alieleza Bw. Julius Agutu.

Aliongeza kwa kusema, "katika kikao kazi hiki cha leo masuala yatakayojadiliwa ni kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za umoja wa wana TSC Mkoa Mara, kupokea taarifa/mrejesho wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu kilichofanyika tarehe 09 Septemba, 2021 na kujadili namna bora ya utekelezaji wa majukumu yetu hususani katika kipindi cha Januari - Juni, 2022."

Mbali na Mkuu huyo wa Wilaya ya Tarime, viongozi wengine waliohudhuria katika kikao kazi hicho ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Tarime (Bw. John Mahinya Marwa), Mwenyekiti wa Chama cha Walimu (CWT) Mkoa wa Mara (Bw. Livingstone Gamba), Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Wilaya ya Tarime (Bw. Matinde Magabe) na Bi. Marina Ngailo (Afisa Elimu Watu Wazima wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime) aliyewawakilisha Maafisa Elimu wa Wilaya ya Tarime.



*Mkuu wa Wilaya ya Tarime Mhe. Luteni Gabriel Mntenjele (aliyekaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali walioalikwa katika kikao kazi cha watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara kilichofanyika tarehe 08/12/2021 Mjini Tarime. Kulia mwa Mkuu wa Wilaya ni Katibu wa CWT Wilaya ya Tarime, Bw. Matinde Magabe, Kaimu Katibu Msaidizi Wilaya ya Tarime, Bw. Julius Agutu, Kaimu Katibu Msaidizi Wilaya ya Musoma, Bw. Samwel Biyani na kwa upande wa kushoto kwa Mkuu wa Wilaya ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Tarime, Bw. John Mahinya Marwa, Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Mara, Bw. Livingstone Gamba na Afisa Elimu Watu Wazima wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Bi. Marina Ngailo*



*Watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mara wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa kikao kazi cha watumishi hao kilichofanyika tarehe 08/12/2021 Mjini Tarime.*

# PROF. KOMBA: TUTAENDELEA KUTOA MAFUNZO KWA KAMATI ZA WILAYA, WATUMISHI NA WALIMU



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akifunga Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Mmoja wa Wajumbe wa Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini akitoa neno la shukrani wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu.**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba amesema kuwa utoaji wa mafunzo ni moja ya vipaumbele vya TSC katika kuhakikisha Watumishi wa Tume hiyo, Kamati za Wilaya pamoja na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanatekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi.

Profesa Komba ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alieleza kuwa TSC iliamua kutoa mafunzo kwa kamati za Wilaya baada ya kugundua kuwa kuna udhaifu katika kutoa haki kwa walimu hususan katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na alieleza kuwa udhaifu huo unasababishwa na Wajumbe wa Kamati hizo kutokuwa na uelewa wakutosha katika sheria.

"Tumejikita katika kutoa mafunzo kwa kamati za TSC Wilaya ili kuwaongezea ujuzi wa kutenda haki hususan wakati wa kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu kwani tumegundua kuwa kuna ukiukwaji mwingi wa taratibu unaofanywa na kamati hizi



*Mmoja wa washiriki wa Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini akiwa anachangia mada wakati wa mafunzo hayo.*

# PROF. KOMBA: TUTAENDELEA KUTOA MAFUNZO KWA KAMATI ZA WILAYA, WATUMISHI NA WALIMU

kutokana na kutokujua sheria na kanuni zake," alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema suala la mafunzunzo sio tu kwamba ni muhimu Kamati za Wilaya peke yake lakini pia tume hiyo inaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake hususan katika eneo la utafiti ili waweze kuetekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi.

"Hatulengi kutoa mafunzo kwa kamati za Wilaya tu, hapana! Tunalenga pia kuwajengea uwezo watumishi wetu kwani kama mnavyofahamu moja ya majukumu ya TSC kwa mujibu wa sheria ni kumshauri Waziri mwenye dhamana juu ya masuala ya elimu na walimu. Ili tuweze kumshauri ni lazima tufanye tafiti, ndiyo maana tunaona kuna umuhimu mkubwa kuwajengea uwezo watumishi wetu ili waweze kumudu masualala ya tafiti," alieleza.

Kiongozi huyo alikwenda mbali zaidi na kueleza kuwa TSC pia inajipanga kuona namna inavyoweza kutoa mafunzo kwa walimu ili waweze kuetekeleza majukumu yao ipasavyo hususan katika kuwalea wanafunzi kiroho.





*Baadhi ya washiriki wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kufunga Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

Alifafanua kuwa kwa kiasi kikubwa walimu wamejikita zaidi katika kuwalea watoto kitaaluma lakini malezi ya kiroho yamesahaulika kwa kitu ambacho kinasababisha kuwepo kwa mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii.

"Tunaona kwamba kwenye elimu yetu, walimu wanasoma vyuoni lakini hatuoni matunda mazuri hasa inapokuja suala la kuwalea watoto kiroho. Tunataka mwanafunzi anapopita kwenye mikono ya mwalimu asibubiri hadi shehe au mchungaji amfundishe ndio awe bora kimaadili, siyo lazima aende kanisani au msikitini kujua kipi ni kizuri na kipi ni kibaya," alisema Prof. Komba.

Aliendelea kusema kuwa kwa kutumia mitaala iliyopo sasa, walimu bado wanaweza kuwabadilisha wanafunzi kiroho na wakawa raia wema wenye maadili yanayohitajika katika jamii badala ya kujikita katika kuinua taaluma za wanafunzi peke yake.

"Mwanafunzi akibadilika katika nyanja moja tu ya taaluma bado haitoshi. Lengo letu ni kuona kadiri mwanafunzi anavyokuwa na maendeleo katika taaluma yake, tuone pia anakuwa na maendeleo chanya katika tabia na maadili kwa ujumla. Mwanafunzi anayebadilika katika nyanja moja tu ya taaluma anakuwa bado hajakamilika," alisema.

# TSC MBEYA: WAKUU WA SHULE WANAHITAJI MAFUNZO WATEKELEZE MAJUKUMU YAO KWA WELEDI

**Na Mwandishi Wetu.**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbeya, Efraim Kamendu ameshauri TSC Makao Makuu kuweka Mkakati Madhubuti wa kutoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuwa ndiyo Mamlaka ya kwanza ya Nidhamu kwa Walimu.

Kamendu ametoa ushauri huo hivi karibuni wakati Jarida la Sauti ya TSC lilipofika ofisini kwake na kufanya mahojiano maalumu kwa lengo la kujua utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbeya, Efraim Kamendu akiwa ofisini kwake wakati wa mahojiano maalum na Jarida la Sauti ya TSC yaliyofayika hivi karibuni jijini Mbeya.*

Alieleza kuwa kuna baadhi ya Wakuu wa Shule wanafanya vizuri katika kusimamia nidhamu ya walimu lakini wengi wao bado hawajafanya kazi hiyo kikamilifu kutokana na kutokuwa na uelewa mpana wa masuala ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na kutotaka kuonekana wabaya kwa walimu wanaowaongoza.

"Wapo ambao wanafanya vizuri katika kuwachukulia hatua walimu pale wanapokiuka maadili ya kazi, lakini wengi wao ni waoga na hawataki waonekane wabaya kwa walimu. Hii imefanya baadhi yao kutuletea kesi za walimu ambazo kwa mujibu wa sheria wanapaswa kuzishughulikia wao wenyewe", alisema Kamendu.

Alifafanua kuwa kwa upande wa Ofisi yake wamejitahidi kuwaelekeza na kuwapatia nyenzo mbalimbali za kufanyia kazi Wakuu hao wa Shule ili watekeleze majukumu yao kwa weledi lakini anaona bado kuna haja ya kupatiwa mafunzo zaidi na kufafanuliwa vizuri sheria ya TSC na Kanuni zake.

Aliongeza kuwa kwa kuwa TSC Makao Makuu imekuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa Watumishi wake na Kamati za Wilaya, ni vyema pia kuona umuhimu wa kuandaa mafunzo kwa ajili ya Wakuu wa Shule na kuwaelekeza Sheria Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu



*Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Wilaya ya Mbeya, Adrophina Mwalingo akiwa ofisini kwake.*

# TSC MBEYA: WAKUU WA SHULE WANAHITAJI MAFUNZO WATEKELEZE MAJUKUMU YAO KWA WELEDI

na Utumishi wa Umma.

"Sisi tunajitahidi kuwaelekeza na kuwapatia miongozo ya kazi lakini bado haitoshi. Ukiangalia kwa mfano, juzi tulikuwa Dodoma kwenye Mafunzo ya Kamati za Wilaya, yale yana msaada mkubwa kwetu kwa kuwa tunakutana na wataalam waliobobea katika Nyanja zote za kiutumishi. Sasa Kama Wakuu wa Shule nao wangepata mafunzo kama yale ninaamini utendaji wao ungebadilika sana," alisema.

Kiongozi huyo alieleza kuwa changamoto anayoina kwa sasa kwa walimu wilayani hapo ni suala la ulevi hususani kwa baadhi ya wale wanaofanya kazi maeneo ya vijijini ambao wameiga tabia za jamii hizo na kujikuta wakikiuka maadili ya utumishi wao.

Alisema pamoja na kuwa changamoto hizo zipo kwa kiwango kidogo Wakuu wa Shule hawajachukua hatua zinazotakiwa kwa kuwa wanaogopa kuonekakana wabaya kwa walimu kitu ambacho kinafanya tabia hizo ziendee.

Alisema kuwa ofisi yake inaelekeza nguvu katika kutoa elimu kwa walimu ili kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa na kwa wale ambao hawatakuwa tayari kubadilika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448.

Ofisi ya TSC Wilaya ya Mbeya ni moja ya Ofisi za TSC zinazohudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmasahuri ya Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kwamba changamoto kubwa iliyokuwa inawakumba walimu kwa miezi michache iliyopita ilikuwa ni kukaa muda mrefu kazini bila kupandishwa vyeo.

Hata hivyo anaeleza kuwa kero hiyo imekwisha baada ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kuamua watumishi hao wapandishwe madaraja ambapo jumla ya walimu 1190 wa Halmashauri ya Jiji na walimu 713 wa Halmashauri ya Wilaya walipandishwa.

Aliongeza kuwa walimu wote waliokuwa na sifa za kupanda walipandishwa na wale ambao walionekana kutopandishwa kwa muda mrefu kwa kipindi cha nyuma wamekuwa wakiombewa kibali maalum kwa Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na wamekuwa wakipandishwa kwa mserereko hadi kufikia madaraja wanayostahili.



*Mafunzo ya Kamati za TSC Wilaya yaliyofanyika hivi Karibuni Jijini Dodoma na kuwakutanisha Wajumbe wa Kamati kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Mbeya, Efraim Kamendu ameyaelezea kuwa yana tija kubwa katika utendaji wa kazi za Kamati hizo.*

# TSC YAPEWA RAI KUTOA MAFUNZO YA AWALI YA NIDHAMU, MAADILI YA UALIMU NA UTUMISHI WA UMMA KWA WALIMU WENYE SHAHADA KABLA YA KURIPOTI VITUO VYA KAZI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi zinazojumuisha mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Songwe, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi wametoa rai kwa Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu kuwapatia mafunzo ya awali ya uelewa juu ya nidhamu, maadili ya ualimu na utumishi wa umma kwa walimu wenye shahada ya ualimu kutokana na hali yao ya nidhamu kutiliwa shaka mara wanaporipoti maeneo yao ya kazi.

Rai hiyo ilitolewa hivi karibuni na Wajumbe wa Kamati hizo za Wilaya wakati wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe hao juu ya utendaji kazi wa Kamati za Wilaya katika maeneo yao yaliyofanyika Mkoani Dodoma wakibainisha kuwa idadi kubwa ya walimu wenye shahada za ualimu tofauti na wale wa daraja 'A' wamekua na nidhamu zinazokinzana na maadili ya ualimu na utumishi wa umma.



*Washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi wakiwa wanapewa mafunzo juu ya Maadili ya Kazi ya Ualimu kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Maadili na Nidhamu wa TSC, Robert Lwikolela.*

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli, akifungua mafunzo hayo alitoa wito kwa walimu wote nchini kuwa chachu ya kuliwezesha Taifa kuwa na watu wenye nidhamu na maadili kwa kutekeleza na kusimamia vema elimu ya msingi na sekondari kama Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na maadili katika Utumishi wa Umma zinavyoelekeza.

Aidha, Mweli aliainisha kuwa hadi kufikia mwezi Oktoba, 2021 Taifa lina jumla ya walimu 258,291 ambapo kati yao 173,591 ni walimu wa shule za msingi na 84,700 wa shule za sekondari wanaohudumiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu, hivyo Kamati hizo za Wilaya za Tume zina wajibu wa kuhakikisha walimu wanapata huduma zinazostahili na kupunguza malalamiko na changamoto mbalimbali miongoni mwao ikiwa ni pamoja na kudumisha nidhamu na maadili katika maeneo yao ya kazi.

Akiwa Mgeni Rasmi akimuwakilisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, OR – TAMISEMI,



*Mmoja wa Washiriki wa washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi akichangia hoja wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga akiwasilisha mada kuhusu Ajira na Maendeleo ya Walimu wakati wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# TSC YAPEWA RAI KUTOA MAFUNZO YA AWALI YA NIDHAMU, MAADILI YA UALIMU NA UTUMISHI WA UMMA KWA WALIMU WENYE SHAHADA KABLA YA KURIPOTI VITUO VYA KAZI

Ummy Ally Mwalimu (Mb), hivi karibuni, Naibu Katibu Mkuu huyo aliwapongeza sana wajumbe wote wateule kwa kuweza kutekeleza majukumu yao tangu kuteuliwa mwezi Mei, 2020 mpaka kupata mafunzo mwezi huu wa Desemba, 2021 ambapo Serikali ina imani baada ya mafunzo hayo wajumbe watatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Alisema, "Wajumbe wote mnaoshiriki katika mafunzo haya mna mchango mzuri wa mawazo ambao utawezesha kuweka mikakati mizuri ambayo itatumika kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kila siku wa majukumu yenu na itasaidia Tume pia kusimamia vyema maadili ya walimu na kuchukua hatua stahiki kwa walimu watakaobainika kukiuka maadili na miiko ya kazi yao."



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*

Nae Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba, alisema tangu kuanzishwa kwa Tume na kuanza kutekeleza majukumu yake mwezi Julai, 2016 Tume imetimiza miaka mitano na miezi sita huku muda uliowekwa Kisheria kwa wajumbe wa Tume na Kamati za Wilaya ni miaka mitatu. Hivyo, Tume iliyopo sasa pamoja na Kamati za Wilaya niza awamu ya pili, baada ya wajumbe wa awali kukamilisha muda wao.

Hali kadhalika, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, pia aliwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wateule wa kamati za wilaya kwa ushirikiano wao na kujitahidi kutekeleza majukumu yao vema licha ya kuwa na majukumu mengine wakiwa pia ni watumishi wa umma katika ofisi zao nje ya majukumu ya Tume na kuwaomba waendeleze moyo huo wa Kizalendo.

Sehemu ya mada zilizowasilishwa katika mafunzo haya ni pamoja na; kusudi la kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, Muundo na Majukumu ya Tume, Majukumu ya Tume kuhusu masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Maadili/ Miiko ya Kazi ya Ualimu, Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu na Taratibu za Uendeshaji wa vikao vya Kamati za Wilaya.



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja kati ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo Elekezi kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wapili kutoka kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kulia) na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa kwanza kushoto).*

# TSC MUFINDI: NIDHAMU YA WALIMU NI NZURI

**Na Mwandishi Wetu.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mufundi imesema kuwa hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo imeimarika kwa kiasi kikubwa kutokanana ofisi hiyo kutoa elimu ya maadili na taratibu za kiutumishi kwa walimu wa Wilaya hiyo.

Kauli hiyo imetolewa na Afisa wa TSC wa Wilaya hiyo, Hellena Mbungu wakati wa mahojiano maalumu na Jarida hili yaliyofanyika hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya maendeleo ya ofisi hiyo katika kusimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali katika Wilaya hiyo.

Alieleza kuwa kitu kinachofanya waone hali ya nidhamu kwa walimu imeimarika ni kupungua kwa kiasi kikubwa cha idadi ya mashauri ya nidhamu katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Desemba 2021.




*Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mufindi, Hellena Mbungu akiwa ofisini kwake wakati wa mahojiano na Jarida hili.*

"Mwaka 2019/2020 tulikuwa na mashauri ya nidhamu 16, mwaka 2020/2021 mashauri yalipungua hadi kufikia 6 na kwa mwaka huu 2021/2022 ambao tumemaliza nusu yake hatuna shauri la nidhamu hata moja. Hii inaonesha kumekuwa na mabadiliko makubwa kwa walimu wetu," alisema.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (kulia) akiwa katika mahojiano maalum na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya Wilaya ya Mufindi, Hellena Mbungu.*

Mbungu aliongeza kuwa katika mashauri yaliyokuwepo miaka iliyopita walimu wengi walikuwa wanashtakiwa kwa makosa ya utoro kazini, ambapo wengi wao walikuwa hawajui umuhimu wa kuzingatia taratibu za kazi na madhara wanayoweza kuyapata pale wanapokiuka taratibu hizo.

"Kwa miaka ya nyuma walimu wengi walikuwa hawazijui sheria na taratibu za utumishi wa walimu vizuri. Wengi wao walikuwa wanaondoka kwenye vituo vya kazi bila ruhusa na walikuwa wanaona ni jambo la kawaida tu bila kujua madhara ya kusa la utoro ni pamoja na kufukuzwa kazi. Ndiyo sababu utaona kwamba katika mashauri ya walimu tuliyokuwa nayo, wengi wao walikuwa na makosa ya utoro kazini," alisema.

Aliongeza kuwa kuimarika

# TSC MUFINDI: NIDHAMU YA WALIMU NI NZURI

huko kwa nidhamu kumetokana na ofisi hiyo kuanza mkakati wa kuwatembelea walimu na kuwaelimisha kuhusu taratibu za kuzingatia katika utumishi wa walimu ili kutojiingiza katika makosa ya nidhamu.

Pamoja na hali ya nidhamu kuwa nzuri, Mbungu anaeleza kuwa ofisi yake ina mpango wa kuweka utaratibu kwa wakuu wa shule ambao ndio mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu ili waweze kuwasilisha taarifa za masuala ya nidhamu katika ofisi hiyo kila mwezi.

"Wakati mwingine yapo mambo yanayoweza kutokea kwenye ngazi ya shule na tusipate taarifa zake, hivyo tunaweka utaratibu ili wakuu wa shule wawe wanatupatia taarifa za masuala ya nidhamu ya walimu wanaowasimiamia. Hii itatusaidia kuona ni sehemu zipi zinachangamoto ili tuongeze nguvu katika kutoa elimu," alisema afisa huyo.

Ofisi ya TSC Wilaya ya Mufindi inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji Mafinga na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ambapo Halmashauri ya mji Mafinga ina walimu 370 wa shule za msingi na walimu 281 wa shule za sekondari huku Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ikiwa na walimu 1284 wa msingi na 683 wa sekondari wanaofundisha shule za Serikali.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (kulia) akiwa katika mahojiano maalum na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya Wilaya ya Mufindi, Hellena Mbungu.*

# KATIBU TSC AMEMPONGEZA NA KUMSHUKURU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI, MHE. JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI (MB), KWA UTEUZI WA KAMISHNA, WAKILI OPTAT JAMES MRINA

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, amempongeza na kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb), kwa kufanya uteuzi wa Kamishna Mteule wa Tume, Wakili Optat James Mrina, kwani ni mkongwe katika utoaji huduma ya Sheria na mwenye weledi wa kutosha katika Sheria na majukumu ya Tume vile amekua akishiriki kama mwalikwa katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama (watatu kutoka kushoto, aliye suka na kuvaa miwani) akiwa katika picha ya pamoja na Kamishna mpya wa TSC wakili Optat James Mrina (mwenye tai ya bluu) wakati Kamishna huyo alipofika ofisi za TSC mara baada ya kuapishwa Novemba 30, 2021 jijini Dodoma, wengine ni baadhi Wajumbe wa Menejimenti ya TSC.*

Katibu huyo wa TSC alitoa pongezi hizo wakati sehemu ya wajumbe wa Menejimenti ya TSC kwa niaba ya Watumishi wote wa Tume walipompokea na kumkaribisha rasmi Ofisi za Tume mara baada ya kiapo kilichofanyika siku za hivi karibuni mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb), akiwa tayari kuanza kazi rasmi akiwa Kamishna Mteule.

Katibu wa TSC Mwl. Nkwama alisema, Tume inahudumia sehemu kubwa ya Watumishi wa Umma ambao ni walimu 258,291 ikiwa walimu 173,591 ni walimu wa Shule za Msingi na walimu 84,700 ni walimu wa Shule za Sekondari ambao wanategemea sana mchango wa huduma za Kisheria katika kushughulikia masuala mbalimbali ya Walimu na Tume kwa ujumla wake.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (aliyekaa mbele) akiwa pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakimkaribisha Kamishna mpya wa TSC, Wakili Optat James Mrina (wa kwanza upande wa kushoto) mara baadya ya kuwasili kwenye ofisi za tume hiyo Novemba 30, 2021.*

Nae Kamishna Mteule Wakili Optat James Mrina akipokea salamu za ukaribisho huo alitoa ahadi kujitahidi kutumia uwezo wake wote kwa kadri awezavyo kutoa ushirikiano wa karibu katika kutekeleza na kutimiza malengo tarajiwa ya majukumu ya Tume ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi shughuli zote zinazoihusu kamati husika ya Kisheria kwa nafasi yake ya uteuzi.

Nae Mkurugenzi wa Huduma za Sheria (TSC), Wakili Richard Odongo, akizungumza kwa niaba ya Watumishi wote wa Tume alimuahidi ushirikiano unaostahili katika kutekeleza majukumu ya uteuzi wake huku akitanabaisha uwazi uliokuwepo awali kabla ya uteuzi wake katika eneo hilo la huduma za Kisheria katika kuwahudumia wateja wa Tume ambao ni walimu na mashauri yao mbalimbali ya kinidhamu na maadili kazini.

# WALIMU WATAKIWA KUSOMA SHERIA YA TSC NA KANUNI ZAKE ILI KUJUA WANACHOPASWA KUFANYA



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea katika mkutano wa viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa Jiji la Mbeya (hawapo pichani) uliofanyika hivi karibuni jijini Mbeya.*



*Kamishna wa TSC, Huruma Mageni akiongea katika mkutano wa viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa Jiji la Mbeya (hawapo pichani) uliofanyika hivi karibuni Jijini Mbeya.*



*Kamishna wa TSC, Jane Mtindya akiongea katika mkutano wa viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa Jiji la Mbeya (hawapo pichani) uliofanyika hivi karibuni Jijini Mbeya.*

**Na Mwandisha Wetu.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amewataka walimu kusoma na kuelewa Sheria na Kanuni za Tume ya Utumishi Walimu ili wasijiingize katika makosa ya kinidhamu wakati wanapotekeleza majukumu yao.

Nkwama ametoa kauli hiyo hivi karibuni katika mkutano uliowakutanisha viongozi wa TSC na walimu wa Shule za Msingi na Sekondani wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya uliofanyika katika Ukumbi wa Shule ya Msingi na Sekondari ya Aggrey iliyoko mkoani Mbeya.

Katibu huyo alisema kuwa baadhi ya walimu wamejikuta wakifanya makosa ya kinidhamu kwa kutokujua taratibu, hivyo ni muhimu kwa kila mwalimu kutumia muda wake kusoma nyaraka hizo ili kujua kile anachopaswa kuetenda na kile ambacho hapaswi kutenda.

"Ninawasihi msome sheria na kanuni ili mfahamu nini mfanye na nini msifanye. Sasa hivi tunaendelea na utaratibu wa kutafsiri sheria zetu kutoka lugha ya Kiingereza kuja katika lugha ya Kiswahili ili kila mmoja aweze kuzielewa. Lakini hata kabla hatujakamilisha mchakato huo ninawaomba pitieni kwenye tovuti ya Tume ambayo ni www.tsc.go.tz mtazipata," alisema.

Akiendelea kufafanua,



*Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo akiongea katika mkutano wa viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa Jiji la Mbeya (hawapo pichani) uliofanyika hivi karibuni jijini Mbeya.*



*Maafisa kutoka TSC Makao Makuu, Julius Mshana (kulia) na Pastory Munyaki wakiwa katika mkutano uliowakutanisha viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa Jiji la Mbeya (hawapo pichani). Mkutano huo ulifanyika hivi karibuni Jijini Mbeya.*



*Mmoja wa walimu wa Jiji la Mbeya akiuliza swali katika mkutano uliowakutanisha viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa jiji la Mbeya.*

# WALIMU WATAKIWA KUSOMA SHERIA YA TSC NA KANUNI ZAKE ILI KUJUA WANACHOPASWA KUFANYA

Nkwama alieleza kuwa baadhi ya walimu wamekuwa wakijihusisha na makosa ya utoro kazini bila kuelewa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, kosa la utoro kazini kwa zaidi ya siku tano mfululizo adhabu yake ni moja tu, kufukuzwa kazi.

"Ninaomba niwaeleze kuwa kosa la utoro kazini linaongoza katika makosa yote yanayofanywa na walimu. Na baadhi yenu hamuelewi kwamba ukipatikana na hatia ya kosa la utoro kazini kwa zaidi ya siku tano mfululizo hakuna adhabu mbadala zaidi ya kufukuzwa kazi. Hivyo pale unapokuwa na shida omba ruhusa, usitoke kwenye kituo chako cha kazi bila kupata ruhusa," Nkwama alisisitiza.

Hata hivyo Katibu huyo aliwaeleza walimu kuwa kuwepo shuleni peke yake bila kutimiza majumu yao kikamilifu bado ni kosa kwa mujibu wa sheria, hivyo kila mwalimu anapaswa kuhakikisha anatimiza wajibu wake kama anavyopangiwa na mkuu wake wa kazi.

Aliongeza kuwa pamoja na jukumu la kufundisha, mwalimu ana wajibu wa kumlinda mwanafunzi dhidi ya mazingira yote yanayoweza kuhatarisha usalama wake na kuhakikisha muda wote mwanafunzi akiwa shuleni hapati tatizo lolote.

"Baadhi ya walimu wanafikiri wakishaingia darasani wakafundisha, wakatoa mazoezi na kusahihisha basi wamemaliza kazi, hiyo sio sawa. Mwalimu una wajibu wa kuhakikisha mwanafunzi yupo katika mazingira salama wakati wote akiwa shuleni. Hilo naomba kila mmoja wetu ajue kuwa ni jukumu lake na lipo kwenye Nguzo za Maadili ya Kazi ya Ualimu," alisema.

Hata hivyo, Nkwama aliwapongeza walimu kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi kitu ambacho kimeendelea kufanya kiwango cha ufuaulu kuongezeka katika Mitihani ya Taifa ya Shule za Msingi na Sekondari nchini.

Kwa upande wake Kamishna wa TSC, Huruma Mageni ambaye alimwakilisha Mwenyekiti wa TSC kwenye mkutano huo, alisema kuwa TSC imekuwa na utaratibu wa kukutana na walimu mara kwa mara kwa lengo la kuwakumbusha kuzingatia maadili ya kazi ya walimu pamoja na kujibu hoja zao ili kuhakikisha mwalimu anatekeleza wajibu wake akiwa na amani.

"Tunapokutana na kuongea nanyi, hata sisi wenyewe kazi yetu inakuwa rahisi kwa kuwa kupitia mikutano hii elimu mnayoipata inasaidia msiingie katika makosa ya kinidhamu. Tunatoa elimu kwa kuwa hatupendi mwalimu yeyote aharibikiwe katika utumishi wake, hatupo kwa ajili ya kufukuza kazi walimu wala hatupendi kuona mwalimu anaondoka katika utumishi wake kwa kufukuzwa kazi," alisema Mageni.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo alisema kuwa Tume hiyo inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu huku akisisitiza kuwa kila wakati wamekuwa wakijitahidi kutenda haki katika kuamua masuala mbalimbali ya walimu.

"Hatufanyi kazi kwa utashi wetu, wakati wote tunafanya kazi kwa mujibu wa sheria, ni kweli kwamba hatupendi kumfukuza kazi mwalimu lakini pale anapokutwa na hatia tunaangalia sheria inasemaje na sheria peke yake ndiyo inayoamua," alisema Odongo.

Katika mkutano huo walimu walipata fursa ya kuwasilisha hoja zao na kuuliza maswali mbalimbali ambayo yote yalitolewa majibu na viongozi hao.



*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi, Lameck Mbeya (kulia), Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Grace Mrema (katikati) na Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga wote kutoka TSC Makao Makuu wakiwa katika mkutano uliowakutanisha viongozi wa TSC na baadhi ya walimu wa Jiji la Mbeya (hawapo pichani). Mkutano huo ulifanyika hivi karibuni Jijini Mbeya.*



*Badhi ya Walimu wa Jiji la Mbeya waliohudhuria Mkutano wao na viongozi wa TSC Makao Makuu.*

# KUTOKUWEPO KWA RUFAA ZILIZOKATWA ZA MASHAURI YA NIDHAMU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU MFULULIZO KWABAINISHA KUIMARIKA KWA HALI YA NIDHAMU ZA WALIMU WILAYANI MBARALI

**Na. Mwandishi Wetu – Mbarali, Mbeya**

Imebainika kuimarika kwa hali ya nidhamu za walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya baada ya kutokuwepo kwa rufaa yoyote ya shauri la nidhamu iliyokatwa katika ngazi ya wilaya hiyo kwa kipindi cha mwaka 2018/19, 2019/20, 2020/21, na 2021/22 ikiwa ni kipindi cha nusu mwaka sasa cha utekelezaji wa majukumu ya Mwaka wa Fedha 2021/ 2022.

Hali hiyo ilibainika hivi karibuni wakati wa mazungumzo ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara zake za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya na Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mbarali, Ndg. Shemgei Shehagilo, ikiwa ni mwendelezo wa ziara hizo za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya zipatazo 139 hapa nchini ili kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC.

"Kwa kipindi cha nyuma kuanzia mwaka 2018/2019 tumekua tukipokea mashauri yasiyozidi 13, yakashuka mpaka matatu na yasiyozidi matano kwa mwezi, baadae yakashuka mpaka kuwa tunapokea shauri moja kwa mwezi, na sasa tangu kuanza kwa mwaka huu wa fedha 2021/ 2022 ambao sasa Desemba hii, 2021 ni robo ya pili ya utekelezaji kwa maana ya nusu mwaka sasa, hatujapokea shauri hata moja la nidhamu hapa wilayani. Hii ni ishara tosha kuwa hali ya nidhamu imeimarika na walimu wanafuata



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbarali, Shemgei Shehagilo (kulia) akiwa katika mahojiano maalum na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami.*

# KUTOKUWEPO KWA RUFAA ZILIZOKATWA ZA MASHAURI YA NIDHAMU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU MFULULIZO KWABAINISHA KUIMARIKA KWA HALI YA NIDHAMU ZA WALIMU WILAYANI MBARALI




*Jengo la Mkuu wa Wilaya ya Mbalali ambapo ndizo ilipo ofisi ya TSC ya Wilaya hiyo.*

maadili ya kazi ya ualimu na utumishi wa umma kwa ujumla wake." Alisema Ndg. Shehagilo

Ndg. Shehagilo alisema mafanikio hayo na hali hiyo yanachagizwa na ushirikiano mkubwa na mzuri uliopo baina ya Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule wanazohudumia kunakoleteleza kuombwa kuhudhuria mikutano na vikao mbalimbali vya walimu ambapo huombwa kuwasilisha mada za uelimishaji juu ya ajira, nidhamu, maadili, na maendeleo ya walimu ambayo ndiyo majukumu mahsusi ya TSC.

Aidha, KKM Shehagilo alisema hali hiyo imechangia pia kuongeza ufaulu wa jumla kuwa mzuri na kuvuka kiwango cha malengo ya Kitaifa katika ufaulishaji inayofikia kati ya asilimia 87 hadi 91 ambapo nyuma ya mafanikio hayo ni nidhamu bora na kufuata maadili.

Pamoja na mafanikio hayo alitoa shukrani kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbarali na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa ushirikiano wao mzuri na mkubwa kiuwezeshaji kiuchumi na usafiri pale inapolazimu nje ya uwezeshaji wa ndani wa TSC ili kufikia malengo ya utoaji huduma bora kwa walimu wilayani na kuondoa malalamiko.

Ofisi ya TSC Wilayani Mbarali, Mkoani Mbeya inahudumia Halmashauri moja ya Wilaya ya Mbarali ikiwa na jumla ya shule 142 ambazo kati yake Shule za Msingi ni 116 na Sekondari 26 zikihudumiwa na jumla ya Walimu 1,736 ambao kati yao; Walimu 1,204 wanafundisha Shule za Msingi wakiwa ni wanaume 595 na Wanawake 609 huku Walimu 532 wakiwa wanafundisha Shule za Sekondari ambao Wanaume ni 376 na Wanawake 156.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akiwa katika studio Redio Mafinga Fm iliyopo wilayani Mufindi. Kiongozi huyo alifanya ziara katika kituo hicho cha redio kwa lengo la kutafuta vipindi kwa ajilinya Kaimu Katibu Wasaidizi kuelimisha Umma juu ya TSC na Majukumu yake.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akiwa katika studio Redio Mafinga Fm iliyopo wilayani Mufindi. Kiongozi huyo alifanya ziara katika kituo hicho cha redio kwa lengo la kutafuta vipindi kwa ajilinya Kaimu Katibu Wasaidizi kuelimisha Umma juu ya TSC na Majukumu yake.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akiwa katika studio Redio Mafinga Fm iliyopo wilayani Mufindi. Kiongozi huyo alifanya ziara katika kituo hicho cha redio kwa lengo la kutafuta vipindi kwa ajilinya Kaimu Katibu Wasaidizi kuelimisha Umma juu ya TSC na Majukumu yake.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akiwa katika studio Redio Mafinga Fm iliyopo wilayani Mufindi. Kiongozi huyo alifanya ziara katika kituo hicho cha redio kwa lengo la kutafuta vipindi kwa ajilinya Kaimu Katibu Wasaidizi kuelimisha Umma juu ya TSC na Majukumu yake.*

# TSC - CHUNYA YAJIVUNIA WALIMU WENYE NIDHAMU, KUJITUMA, KUZINGATIA MAADILI YA KAZI NA NGUZO KUU ZA UALIMU



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), George Kanyeka akiwa ofisini kwake.*

**Na. Mwandishi Wetu – Chunya, Mbeya**

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Chunya, Mkoani Mbeya inajivunia kuwa na walimu wenye nidhamu, wanaofuata maadili ya kazi yao na wenye kujituma katika kufundisha na kuwalea wanafunzi katika nguzo kuu za ualimu pamoja na ikama yao kutolingana na uwiano wa idadi ya watoto wanaowahudumia.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Chunya, Ndg. George Kanyeka, wakati alipokua akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara zake za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya zipatazo 139 hapa nchini ili kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC.

Alisema, "Hata kama ikama yetu ya walimu hapa wilayani haitoshi ukilinganisha na idadi ya wanafunzi tunaowahudumia, Walimu wa Chunya ninaowahudumia hapa kwakweli ni wenye nidhamu, wenye kufuata maadili ya kazi yao, na wenye kujituma katika kazi yao ya ufundishaji na malezi ya watoto wanaowahudumia kwa kuzingatia nguzo kuu tano za ualimu. Kwakweli katika hili nawasifu, nawapongeza, na ninajivunia sana hali hii."

KKM Kanyeka alisema pamoja na kujivunia huko walimu wa wilaya yake wanakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo; upungufu wa nyumba za makazi ya walimu kwenye vituo vyao vya kazi, ukosefu wa miundombinu rafiki hasa ya barabara za kutoka kwenye vituo vyao vya kazi mpaka wilayani kupata huduma za mambo mbalimbali yanayowahusu kiutumishi, kutolipwa kwa wakati madeni ya stahiki zao mbalimbali na hasa mishahara, pamoja na kuwa na idadi ndogo ya walimu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi.

Aidha aliongeza kuwa kutokana na ushirikiano na uhusiano mzuri uliopo baina ya ofisi yake na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na hali nzuri ya nidhamu za walimu; zoezi la kuwapandisha vyeo/ madaraja walimu wilayani humo lilikwenda vizuri na kuwezesha jumla ya walimu 345 waliotekeleza vema wajibu wao na kustahili kupandishwa vyeo walipandishwa, ambapo kati yao walimu 211 ni kutoka Shule za Msingi, na walimu 134 niwa Shule za Sekondari wilayani humo.

Ofisi ya TSC Chunya mkoani Mbeya inahudumia Halmashauri moja ya Wilaya ya Chunya ikiwa na jumla ya shule 87 ambazo kati yake Shule za Msingi ni 73 na Sekondari 14 zikihudumiwa na jumla ya walimu 787 ambao kati yao Walimu 570 wanafundhisha Shule za Msingi na 217 wanafundisha Shule za Sekondari.



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***